# LEARNING BY EAR

## MASUALA YA AFYA NA JAMII



### USAFI
Iwe nyumbani, shuleni au katika jamii – mara nyingine inahitaji hatua chache tu kuwa na afya bora.
2010 | RADIO DRAMA



### WATU WENYE ULEMAVU
Oluanda ni mmoja kati ya vijana wengi wanaoishi na ulemavu Afrika. Hata hivyo ana bidii na ari ya kuzitetea haki za watu wenye ulemavu. Sikiliza ili uyafahamu mafanikio yake.
2010 | RADIO DRAMA



### UZAZI WA MPANGO
Jifunze mengi kuhusu uzazi wa mpango na athari zake katika jamii ya Kiafrika. Andamana na wasichana wawili chipukizi wanapopitisha uamuzi wa kuyabadili maisha yao.
2009 | RADIO DRAMA



### MALARIA
Jiunge na familia ya Kiafrika katika harakati zake za kuangamiza Malaria, mojawapo ya magonjwa hatari barani Afrika. Jifunze kuhusu tiba iliyopo na jinsi wanavyoweza kujikinga katika siku za usoni.
2009 | RADIO DRAMA



### WASICHANA
Kuwa mwanamke barani Afrika aghalabu ni jambo zito. Jee, wasichana wanaweza vipi kujiimarisha? Haki zao ni zipi? Andamana na Bibiy katika maisha yake anapowasaidia maswahiba wake kupambana na changamoto za kila siku.
2008 | RADIO DRAMA



### UKIMWI
Sikiliza ujifunze kuhusu virusi vya HIV wakati msichana chipukizi anapopata mimba na kulazimika kupimwa virusi. Jifunze ufumbuzi uliopo anapoondoa hofu na kutafuta ushauri.
2008 | RADIO DRAMA



### AFYA BORA
Shiriki katika pilka pilka za vijana wanaotambua umuhimu wa kuishi katika mazingira safi. Ni rahisi kuwa na afya - pata ushauri unapoisikiliza hadithi yao.
2008 | RADIO DRAMA

## ELIMU YA KAWAIDA



### TAMTHILIA ZINAZODUMISHA UTAMADUNI WA AMANI
Tamthilia huburudisha, husikitisha, hutatiza na pia huchangamsha na kuwavutia wasikilizaji wa vizazi vyote. Hadithi zetu zinavutia na zina ujumbe muhimu kuhusu kuheshimiana na kuvumiliana.
2010 | SPECIAL FORMAT



### KUTOJUA KUSOMA NA KUANDIKA
Ungana na msichana mmoja anayejitahidi kuendelea na masomo katika jamii ambayo watoto wa kiume ndio wanaopewa umuhimu zaidi. Wakati huo huo, wazazi wake wanaanza kuelewa umuhimu wa kujua kusoma na kuandika.
2010 | RADIO DRAMA



### HISTORIA YA AFRIKA
Funga safari ujifunze historia ya kuvutia ya bara lako na ugundue vipi inavyochangia katika maisha yako ya kila siku.
2009 | RADIO DRAMA



### MBINU MPYA ZA MAWASILIANO
Andama na kundi la wafanyabishara chipukizi wanapofungua biashara mpya ya mawasiliano. Wanataka kufungua mkahawa wa intaneti lakini mambo si rahisi. Jee, watafanikiwa kuviondoa vikwazo?
2009 | RADIO DRAMA



### KOMPYUTA NA INTANETI
Ungana nasi wakati marafiki zetu wawili wanapofanya mazungumzo ya kusisimua na kompyuta. Ujue ulimwengu wa kusisimua wa mtandao wa intaneti, elimu kupitia mtandao, muziki na mengine mengi!
2008 | RADIO DRAMA AND FEATURES



### KAZI NA MAFUNZO
Jifunze aina mpya za kazi wakati watalaamu chipukizi wanapoelezea kuhusu ajira zao. Halafu shiriki katika safari ya msichana mmoja wa kijijini anayesomea katika chuo kikuu cha mjini. Ifuatilie hadithi yake ujue kitakachomsibu.
2008 | FEATURES AND RADIO DRAMA



### ELIMU YA KAWAIDA
Kutana na vijana wawili wadogo wanaojaribu kupata maelezo ya masuala tete ya maisha ya kila siku. Jifunze jinsi ya kutuma na kupokea ujumbe mfupi na kinachoisababisha radi. Na jee, ipi siri ya kupendana?
2008 | RADIO DRAMA

## SIASA NA JAMII



### MJADALA WA KIDINI
Mapenzi humwia mhusika vigumu dini inapokuwa kikwazo. Jiunge nasi usikie jinsi tatizo hili linavyogeuka kuwa fursa ya kuendeleza stahamala na maelewano katika hadithi hii kuhusu vijana wawili, wandani wao na familia zao.
2010 | RADIO DRAMA



### SOKA BARANI AFRIKA
Kwa mara ya kwanza bara la Afrika limekuwa mwenyeji wa kinyang'anyiro cha kandanda, na hadithi hii inayaweka yote bayana kuwa kuna mengi zaidi ya kuchuana: ufisadi na rushwa na uhamiaji una mchango mkubwa.
2010 | RADIO DRAMA



### UHAMIAJI
Wahamiaji kutoka kote barani Afrika wana mengi ya kusimulia kuhusu hadithi zao binafsi. Andamana nao katika safari zao hatari za kuelekea Ulaya, zijue changamoto za maisha yao na sababu zilizowafanya baadhi yao kurejea.
2009 | FEATURES



### HABARI NA MAWASILIANO
Ungana na maswahiba wetu vijana wanapojaribu kuanzisha kituo chao cha redio na utambue hali halisi katika sekta ya habari na mawasiliano. Jee, watafanikiwa?
2009 | RADIO DRAMA



### HAKI ZA WATOTO
Katika makala hii, watoto wa Kiafrika wanazitetea haki zao. Kutana na mashujaa wetu vijana wanaposimulia hadithi zao kuhusu changamoto zinazowakabili.
2009 | FEATURES



### WATU WANAOLETA MABADILIKO
Jee, unataka kuisaidia nchi yako na ulete mabadiliko? Tunawatambulisha baadhi ya Waafrika wanaojitolea maisha yao kuwasaidia wengine. Sikiliza wanachokifanya na vipi walivyofaulu.
2009 | FEATURES



### MAKUNDI YA KIJAMII
Makundi ya kijamii yana mchango muhimu katika masuala ya haki na kuboresha hali ya maisha kwa watu wote. Gundua jinsi watu waliojitolea kwa dhati wanavyolitetea bara lao.
2008 | FEATURES



### KUSHIRIKI KATIKA SIASA
Ndugu watatu wanafuatilia ndoto zao za uongozi. Vioja mbalimbali vya kisiasa vyajitokeza katika juhudi zao. Jee, watafaulu kuyafikia malengo yao?
2008 | RADIO DRAMA

## UCHUMI NA MAZINGIRA



### UHAMIAJI MIJINI
Baada ya kukerwa na uhaba wa nafasi za kujiimarisha mijini, vijana waliohitimu katika chuo waamua kuanzisha shirika la kilimo kijijini mwao.
2010 | RADIO DRAMA



### UCHUMI
Ungana na pacha walio na umri wa miaka 16 wakati wanapojitosa katika ulimwengu wa biashara. Yagundue mawazo yao ya ubunifu wanayoyatoa. Wanakabiliana na vikwazo vipi? Watafaulu?
2009 | RADIO DRAMA



### MABADILIKO YA HALI YA HEWA
Kutana na kundi la vijana waliodhamiria kupambana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa. Yafahamu mabadiliko ya hali ya hewa na vipi yanavyokiathiri kijiji chao. Ungana nao katika juhudi zao za kutafuta ufumbuzi bora zaidi.
2009 | RADIO DRAMA



### MAZINGIRA
Andamana na vijana wetu watatu wanapotambua kwamba mazingira yako hatarini – hata barani Afrika. Sikiliza mchezo huu wa redio na ujifunze jinsi ya kuilinda pepo iliyo hatarini.
2008 | RADIO DRAMA



### UTANDAWAZI
Ungana na watangazaji wetu wawili wakati wanapojiandaa kufichua athari za utandawazi katika uchumi wa Afrika. Wape nafasi wakutembeze katika mataifa tofauti barani Afrika ili ujifunze jinsi utandawazi unavyoyaathiri maisha ya watu tofauti.
2008 | FEATURES

Vipindi vyetu vya kuelimisha vya Noa Bongo Jenga Maisha Yako ni mkusanyiko wa michezo ya redio na makala na hupatikana kwenye CD. Kila CD ina vipindi 10 vya kila mchezo. Kila kipindi kina urefu wa dakika 12.



DEUTSCHE WELLE